# SAUTI YA TSC


TOLEO NA.2 JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC) APRILI 2021

Buriani Rais wetu mpendwa

## Hayati John Pombe Joseph Magufuli

## 1959 - 2021

***Tutakukumbuka daima***



**MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA**
**Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz**

*Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania* *tumeyautumishiwawalimutanzania*

# WALIMU TUMUENZI RAIS JPM KWA KUYAISHI ALIYOPIGANIA

Taifa letu lingali limegubikwa na simanzi kubwa ya kuondokewa na mpendwa wetu, Rais wa Awamu ya Tano wa nchi yetu, Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli.

Wakati tukiendelea kuomboleza msiba wa Jemedari wetu huyu, ambaye maisha yake na uongozi wake ulijipambanua kuwa wa kuigwa kutokana na kujawa umahiri wa kipekee, ni vyema pia tukatafakari ni kwa namna gani tunapaswa kumuenzi.

Hayati Rais Magufuli alifanya mengi mazuri katika sekta mbalimbali nchini. Kwetu sisi tunaohusika na utumishi wa walimu, hususani walioko katika sekta ya umma, pia tunayo mengi ya kuyaenzi kutoka kwake. Katika hayo mengi aliyoyaelekeza yafanyike wakati wa uhai na uongozi wake, tunaweza kuyajumuisha katika kundi moja la maadili.

Tumuenzi Rais Magufuli kwa kuwa waadilifu katika kazi yetu. Walimu tukiwa waadilifu, tutachangia kwa kiasi kikubwa ubora wa elimu kwa watoto wetu tunaowafundisha kwani matukio kama kujihusisha kimapenzi na wanafunzi pamoja na utoro kazini, ambayo yamekuwa ni mojawapo ya changamoto katika sekta husika, yataondoka.

Yeye akiwa ni Mwalimu, aliuona umuhimu wa vijana wa kitanzania kupata elimu ili waje walitumikie Taifa lao na kusukuma mbele gurudumu la maendeleo. Ndiyo maana alipoingia madarakani mwaka 2015, aliondoa ulipaji wa ada na michango mbalimbali kwa wanafunzi wote wa shule za serikali kuanzia ngazi ya msingi hadi sekondari.

Hivyo basi, ikiwa tutasimama katika maadili kwa kuhakikisha watoto wa Taifa hili, ambao tumepewa dhamana ya kuwalea kielimu na kimaadili, wanapita katika mikono yetu kwa usalama, tutakuwa tumeunga mkono jitihada za Serikali za kuhakikisha wanapata maandalizi mazuri ya kuja kulijenga Taifa letu. Na kwa kufanya hivyo, tutakuwa tumemuenzi kwa vitendo Rais wetu mpendwa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli.

Kwa kuenenda kinyume na hayo, tutakuwa tunachangia kufifisha na kuua kabisa ndoto zake na yale mazuri aliyoanzisha na kuyasimamia katika sekta ya elimu. Wahenga walisema "Ada ya Mja hunena, muungwana ni kitendo." Basi na tumuenzi Rais wetu kwa vitendo. Hilo linawezekana. Tuanze sasa.

BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
Moses Chitama


**Wajumbe**
Christina Hape
Richard Odongo
Revocatus Misonge
Mectildis Kapinga
Lameck Mbeya

**Mhariri Mkuu**
Veronica Simba

**Mhariri Msaidizi**
Adili Mhina

**Msanifu Kurasa**
Lucas Gordon

## KATUNI




**Wasiliana nasi kwa Simu:** 0739-669610 & 0735-255238 **Barua Pepe:** *secretary@tsc.go.tz*
Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, ***S.L.P 353, DODOMA.***

OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)



Mhe. Samia Suluhu Hassan

# PONGEZI

**TUNAKUPONGEZA**
kwa kuapishwa kuwa
**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

***Tunaahidi kukupa ushirikiano katika kutimiza majukumu yako.***

*Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania*   *tumeyautumishiwawalimutanzania*

# CHITAMA ATAKA UNUNUZI WA UMMA UZINGATIE MISINGI YA UADILIFU

**Na Veronica Simba**

Kaimu Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Moses Chitama amewataka watumishi wa Tume hiyo kuhakikisha kuwa ununuzi wote wa umma unafanyika kwa kuzingatia misingi ya uadilifu.

Aliyasema hayo Machi 1, 2021 mkoani Morogoro wakati akifungua mafunzo yanayohusu masuala ya ununuzi na usimamizi wa mikataba kwa Wajumbe wa Menejimenti ya TSC.

Akifafanua, Chitama alieleza kuwa ununuzi wa umma ukifanyika kwa uadilifu, utawezesha kufikia malengo ya Taifa ya kupata thamani halisi ya fedha ya Serikali inayotumika



*Kaimu Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Moses Chitama, akifungua mafunzo yanayohusu masuala ya ununuzi na usimamizi wa mikataba kwa wajumbe wa Menejimenti ya TSC, Machi 1, 2021 mjini Morogoro.*



*Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Lameck Mbeya, akichangia mada wakati wa mafunzo yaliyohusu masuala ya ununuzi na usimamizi wa mikataba kwa wajumbe wa Menejimenti ya TSC, Machi 1, 2021, mjini Morogoro.*



*Mkurugenzi Msaidizi wa Utawala, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Apsa Othman, akichangia mada wakati wa mafunzo yaliyohusu masuala ya ununuzi na usimamizi wa mikataba kwa wajumbe wa Menejimenti ya TSC, Machi 1, 2021, mjini Morogoro.*

# CHITAMA ATAKA UNUNUZI WA UMMA UZINGATIE MISINGI YA UADILIFU



*Baadhi ya washiriki wa mafunzo yanayohusu masuala ya ununuzi na usimamizi wa mikataba kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), wakifuatilia mada zilizokuwa zikiwasilishwa katika siku ya kwanza ya mafunzo hayo, Machi 1, 2021, mjini Morogoro.*

katika ununuzi.

"Ununuzi wa Umma una mchango mkubwa katika maendeleo ya Taifa letu, hasa ukizingatia kuwa takribani asilimia 70 hadi 80 ya bajeti ya serikali, inakwenda katika ununuzi wa vifaa, kazi za ujenzi na huduma mbalimbali. Hivyo ni muhimu ununuzi ufanyike kwa ufanisi," alisisitiza.

Kaimu Katibu aliwakumbusha washiriki wa mafunzo husika kuwa, Serikali imejikita katika kudhibiti matumizi ya fedha za umma, hivyo inafanya kila jitihada katika kuhakikisha kuwa fedha hizo zinatumika kwa ufanisi.

Aidha, alisema kuwa, pamoja na kwamba wapo wataalamu wa ununuzi wanaowajibika moja kwa moja kufanya kazi hiyo, hata hivyo uongozi wa TSC umeona ni vyema kutoa mafunzo husika kwa viongozi na wataalamu wa kada nyingine mbalimbali, hususani wale wanaotoa maamuzi katika hatua mbalimbali za ununuzi.

Alifafanua kuwa mafunzo hayo yatawajengea uwezo viongozi na wataalamu husika, waweze kushirikiana kwa ufanisi katika utekelezaji pamoja na kuepuka hoja mbalimbali za ukaguzi ambazo hujitokeza pale taratibu za ununuzi zisipofuatwa kikamilifu.

Mafunzo hayo ya siku tano, yalitolewa kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma namba 7 ya mwaka 2011, pamoja na Kanuni zake, tangazo la serikali namba 446 la mwaka 2013, ikisomwa pamoja na marekebisho yaliyofanyika mwaka 2016.

Walioshiriki mafunzo hayo ni Menejimenti, Wajumbe wa Bodi ya Zabuni pamoja na Maafisa Ununuzi ambao ndiyo huhusika katika kutoa maamuzi wakati wa shughuli za ununuzi na usimamizi wa mikataba katika Taasisi husika (TSC).

# CHITAMA ATAKA UNUNUZI WA UMMA UZINGATIE MISINGI YA UADILIFU








*Washiriki wa mafunzo yanayohusu masuala ya ununuzi na usimamizi wa mikataba kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), wakifuatilia mada zilizokuwa zikiwasilishwa katika siku ya kwanza ya mafunzo hayo, Machi 1, 2021, mjini Morogoro.*

OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)

# SALAMU ZA PONGEZI



Dkt. Philip Isdor Mpango

**TUNAKUPONGEZA**
**Mhe. Dkt. Philip Isdor**
## Mpango

kwa kuteuliwa na kuapishwa kuwa **Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

*Tunaahidi kukupa ushirikiano katika kutimiza majukumu yako.*

# TSC Singida yapatiwa Ofisi zenye hadhi

**Na Adili Mhina**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Singida, imepata Ofisi zenye hadhi na sasa imeondokana na adha ya kukaa katika jengo chakavu lililokuwa likihatarisha usalama wa watumishi wake.

Akizungumza na Jarida hili hivi karibuni, Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Singida, David Brown alisema kuwa usalama wao ulikuwa hatarini kutokana na jengo walilokuwa wakitumia kuwa chakavu.

Alieleza kuwa kutokana na uchakavu huo wa Ofisi, walimwandikia barua Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida, Rashid Mandoa kuomba TSC ipatiwe ofisi nyingine kutokana na adha iliyokuwa inawakabili.

Alisema kuwa Mkurugenzi huyo aliamua kuwapatia TSC jengo lenye hadhi ambalo lilikuwa linatumiwa na Idara za Sheria, Ukaguzi wa





*Mwonekano wa jengo la ofisi za sasa za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Wilaya ya Singida.*

# TSC Singida yapatiwa Ofisi zenye hadhi

Ndani, Ugavi na Ununuzi ambazo zilihamishiwa sehemu nyingine.

"Tunamshukuru sana Mkurugenzi Mtendaji kwa kutujali na kuamua kuhamisha Idara nyingine ili atupatie sisi jengo hili ambalo lina hadhi ya ofisi ya umma, hapa sasa tunafanya kazi kwa Amani," alisema Brown.

Sauti ya TSC ilitembelea jengo hilo ambalo lina vyumba vinne ambavyo kwa sasa ni Ofisi ya Katibu Msaidizi, Ofisi ya Afisa Nidhamu, Ofisi ya Afisa Ajira pamoja na Masjala na kushuhudia uwepo wa miundombinu ya mtandao jambo ambalo linasaidia ofisi hizo kuongeza kasi ya utendaji kazi.

Aidha, Brown alieleza kuwa baada ya kuhamia katika ofisi hizo, ufanisi wa kazi umeongezeka kwa kuwa wanafanya kazi bila kuwa na mashaka ya usalama wao na kwamba miundombinu iliyopo katika ofisi hiyo inasaidia kurahisisha utendaji wa kazi.

"Tulikuwa tunachelewa sana kutuma taarifa makao makuu kwa kuwa tulikuwa tunalazimika, baada ya kukamilisha kazi, kutafuta sehemu yenye huduma ya mtandao (internet) jambo ambalo lilikuwa linasababisha kuchelewa kutuma taarifa, lakini kwa sasa kazi zetu zinakwenda vizuri na kwa kasi Zaidi," alifafanua Brown.

Itakumbukwa kuwa hivi karibuni Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serilali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde aliagiza Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri zote kuwapatia watendaji wa TSC ofisi zenye hadhi ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.





*Sehemu ya ndani ya ofisi za zamani za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Wilaya ya Singida ikiwa katika hali ya uchakavu.*

# WATUMISHI WANAWAKE TSC WAIPONGEZA SERIKALI

**Na Veronica Simba**

Wafanyakazi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Makao Makuu Dodoma, wameipongeza Serikali kwa kuendelea kuwathamini wanawake na kuwapatia nafasi za uongozi katika nyanja mbalimbali nchini.

Pongezi hizo zilitolewa Machi 8, 2021 jijini Dodoma na Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa TSC, Catherine Kamili, katika maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, ambapo wafanyakazi hao walishiriki katika maandamano yaliyoshirikisha Taasisi mbalimbali za Serikali na binafsi, yaliyoanzia Uwanja wa Jamhuri hadi katika Uwanja wa 'Nyerere Square.'

Akizungumza kwa niaba ya wafanyakazi wanawake wa TSC,






*Wafanyakazi wanawake wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Makao Makuu Dodoma, wakishiriki katika maandamano wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, Machi 8, 2021.*

Kamili aliwataka wanawake wote nchini, husussani watumishi wa TSC, kuendelea kuchapa kazi kwa weledi na kujituma katika kuhakikisha, wanakuwa sehemu ya waleta maendeleo ya jamii na Taifa.

Maadhimisho hayo yaliongozwa na kaulimbiu isemayo "Wanawake katika Uongozi, Chachu kufikia Dunia yenye Usawa."

"

**Wanawake katika Uongozi, Chachu kufikia Dunia yenye Usawa"**

# WATUMISHI WANAWAKE TSC WAIPONGEZA SERIKALI





*Baadhi ya wafanyakazi wanawake wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), wakiungana na wenzao kutoka Taasisi mbalimbali kucheza, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, yaliyofanyika katika Uwanja wa 'Nyerere Square' jijini Dodoma, Machi 8, 2021.*




*Wafanyakazi wanawake wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Makao Makuu Dodoma, wakiwa katika picha ya pamoja, muda mfupi kabla ya kushiriki katika maandamano wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, Machi 8, 2021.*

# WATUMISHI WANAWAKE TSC WAIPONGEZA SERIKALI











*Matukio mbalimbali wakati wafanyakazi wanawake wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Makao Makuu Dodoma, walipoungana na wenzao kutoka Taasisi mbalimbali za Serikali na Sekta Binafsi, kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, Machi 8, 2021.*

# WATUMISHI WANAWAKE TSC WAIPONGEZA SERIKALI












*Matukio mbalimbali wakati wafanyakazi wanawake wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Makao Makuu Dodoma, walipoungana na wenzao kutoka Taasisi mbalimbali za Serikali na Sekta Binafsi, kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, Machi 8, 2021.*

# UTUMISHI WA UMMA UENDANE NA HOFU YA MUNGU – DC BUPILIPILI



*Mkuu wa Wilaya ya Bunda, Mwalimu Lydia Bupilipili (katikati), akifungua kikao kazi cha walimu viongozi, walimu wakuu, wakuu wa shule pamoja na maafisa elimu, kilichofanyika Machi 2 mwaka huu wilayani humo. Kikao hicho kiliratibiwa na Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Bunda.*

**Na Mwandishi wetu**

Mkuu wa Wilaya ya Bunda, Mwalimu Lydia Bupilipili amewaasa watumishi wa umma, hususani kada ya ualimu, kufanya kazi yao huku wakiongozwa na hofu ya Mungu.

Alitoa wito huo Machi 2 mwaka huu, wakati akifungua kikao kazi kilichoandaliwa na Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Wilaya ya Bunda na kuwahusisha walimu viongozi, walimu wakuu, wakuu wa shule pamoja na maafisa elimu wa wilaya hiyo.

Alisema, ikiwa walimu watakuwa na hofu ya Mungu katika kutekeleza majukumu yao, watatenda kazi hiyo kwa upendo na uadilifu, hivyo kuwa chachu ya

# UTUMISHI WA UMMA UENDANE NA HOFU YA MUNGU – DC BUPILIPILI

**“Ninyi walimu viongozi mnatakiwa kuwa mfano kwa walimu walio chini yenu.”**



*Walimu viongozi, wakuu wa shule, walimu wakuu na maafisa elimu kata, wakifuatilia mada zilizokuwa zikiwasilishwa wakati wa kikao kazi kilichoandaliwa na Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Bunda, Machi 2 mwaka huu.*

maendeleo kwa Taifa.

Aidha, Mwl Bupilipili aliwaasa walimu kutojihusisha na mahusiano ya kimapenzi na wanafunzi, ulevi wa kupindukia na uzembe kazini.

“Ninyi walimu viongozi mnatakiwa kuwa mfano kwa walimu walio chini yenu,” alisisitiza.



*Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Wilaya ya Bunda, Mwalimu Magesa Protas, akizungumza wakati wa kikao kazi cha walimu viongozi, walimu wakuu, wakuu wa shule pamoja na maafisa elimu, kilichofanyika Machi 2 mwaka huu wilayani humo.*

Kwa upande wake, Katibu Msaidizi wa TSC Bunda, Mwalimu Magesa Protas, aliwakumbusha walimu kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za kazi hiyo.

“Wakuu wa shule na walimu wakuu, tambueni kuwa ninyi ndiyo mamlaka za nidhamu katika ngazi ya awali, hivyo mnapaswa kushughulikia mashauri yanayohusu makosa mepesi katika vituo vyenu kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu,” alisema Mwl Protas.

Akizungumzia suala la uhusiano mwema kazini, Mwl Protas aliwahimiza walimu kuwa na upendo baina yao na viongozi huku akiwaasa viongozi wote kutenda haki kwa wale wanaowaongoza.

Kikao kazi hicho kilifanyika katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bunda.

# TSC Singida ilivyojizatiti kudhibiti utoro, kughushi

**"Walimu wanatakiwa kukopa kwa malengo maalum, yenye tija na kuwa na uhakika wa kurejesha mkopo wake bila kuathiri utendaji wake wa kazi."**



*Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Wilaya ya Singida, David Brown akitekeleza majukumu ofisini kwake, hivi karibuni.*



*Afisa Ajira na Maendeleo ya Walimu wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Singida, Martha Komu akitekeleza majukumu yake ya kila siku ofisini kwake.*

**Na Adili Mhina**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Wilaya ya Singida ni miongoni mwa ofisi za TSC ambazo zinahudumia zaidi ya Halmashauri moja. TSC Singida inahudumia Halmashauri ya Manispaa ya Singida na Halmashauri ya Wilaya ya Singida.

David Brown ni Kaimu Katibu Msaidizi wa Wilaya ya Singida, anaeleza kuwa wilaya hiyo ina jumla ya walimu 2,392 wanaosimamiwa na ofisi yake. Katika idadi hiyo, walimu 1,125 ni wa shule za Halmashauri ya Manispaa ya Singida na Walimu

# TSC Singida ilivyojizatiti kudhibiti utoro, kughushi

1,267 ni wa shule za Halmashauri ya Wilaya ya Singida.

Brown anaona kuwa hali ya nidhamu kwa Walimu katika Wilaya hiyo ni nzuri na katika kipindi cha miaka mitatu kumekuwa na idadi ndogo ya mashauri ya kinidhamu ya walimu yaliyofunguliwa, kitu kinachoashiria kuwa walimu wengi wanazingatia miiko na maadili ya ualimu.

Akieleza zaidi, Brown anasema hali hiyo kwa kiasi kikubwa imechangiwa na namna Ofisi yake ilivyojidhatiti katika utoaji elimu kwa walimu kuhusu maadili na miiko ya kazi yao.

"Mwaka 2018 kulikuwa na mashauri ya nidhamu 18, mwaka 2019 mashauri 12 na mwaka 2020 mashauri 13 na hadi mwezi machi mwaka huu 2021 tumefungua mashauri matatu tu, hii ni kwa sababu tumewafikia walimu wengi na kuwapa elimu juu ya sheria, kanuni na taratibu za utumishi wao," anasema Brown.

Pamoja na hali ya nidhamu kuwa nzuri, Brown anaona changamoto mbili zinazoibukia kwa walimu ambazo zinahitaji uthibiti wa haraka, ili kuhakikisha walimu wanadumu katika maadili ya kazi wakati wote wa utumishi wao.

Anaeleza kuwa kumekuwa na tatizo la utoro ambapo kwa kiasi kikubwa walimu vijana ndio wanaoongoza huku sababu kubwa ikielezwa kuwa ni kuwa na madeni mengi yanayofanya walimu kukimbia maeneo yao ya kazi kwa kuhofia kudaiwa.



*Afisa Maadili na Nidhamu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Wilaya ya Singida, Boniface Ndege akiwa Masjala, akiendelea kutekeleza majukumu yake, kama alivyonaswa na kamera yetu hivi karibuni.*

"Tuliamua kufuatilia kuona ni kwanini walimu wengi vijana ndio wanaotoroka na ukizingatia wana muda mfupi tu kazini. Tulichokiona ni kwamba walimu wengi hasa hawa vijana wanakopa kupitiliza, wengi wanamatarajio ya kupata mafanikio ya haraka, hivyo wanaamua kukopa bila kuwa na taarifa za kutosha za miradi wanayotaka kuanzisha, na kujikuta pesa yote aliyokopa inapotea," anasema Brown.

Anaongeza kuwa, "Mwalimu anapokuwa na madeni mengi hawezi kuwa na utulivu darasani. Tulikwenda kutembelea shule fulani na tulitumia usafiri wa pikipiki, kuna mwalimu alikuwa anafundisha lakini aliposikia mngurumo wa pikipiki alitaka kutokea dirishani akidhani anayemdai amekuja."

Anasisitiza kuwa suala la kukopa lina miongozo yake kwa mujibu wa kanuni za utumishi ambapo mwalimu hatakiwi kukopa zaidi ya kiwango kilichowekwa na serikali kulingana na mshahara wake.

Brown anashauri kuwa walimu wanapaswa kuzingatia utaratibu pale wanapotaka kukopa fedha. Pia, wanatakiwa kukopa kwa malengo maalum, yenye tija na kuwa na uhakika wa kurejesha mkopo wake bila kuathiri utendaji wake wa kazi.

Changamoto nyingine ni baadhi ya walimu kughushi nyaraka za vibali vya uhamisho

# TSC Singida ilivyojizatiti kudhibiti utoro, kughushi

ambazo kwa kawaida hutolewa na Katibu Mkuu, Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Anaeleza kuwa yapo mashauri kadhaa ambayo yamefunguliwa kutokana na walimu kughushi barua za vibali vya uhamisho wakiwa na lengo la kumdanganya mwajiri ili waweze kuhama vituo vya kazi.

Kwa mujibu wa Brown, Ofisi yake ilitilia shaka uhalali wa barua za vibali vya uhamisho ambazo baadhi ya walimu waliziwasilisha kwa mwajiri. Ndipo mwajiri aliamua kufanya mawasiliano na Katibu Mkuu TAMISEMI na kujiridhisha kuwa baadhi ya walimu wanaghushi barua za vibali vya uhamisho.

"Unajua utaratibu wa kawaida ni kwamba barua ya mwalimu inatumwa kwa mwajiri ili aipitishe na kumkabidhi mlengwa, lakini baadhi ya walimu walikuja na barua zao mkononi wakidai wamezitoa TAMISEMI na kumwomba mwajiri azipitishe ili waweze kuhama, lakini kumbe ni barua walizotengeneza wenyewe," alisema Brown.

Miongoni mwa sababu zinazoelezwa kuchangia walimu kujihusisha na kughushi nyaraka za uhamisho ni pamoja na baadhi ya walimu vijana wenye ndoa changa kutaka kufuata wenzi wao pasipo kujali taratibu zilizowekwa na hata baadhi yao kuwa wakaidi pale wanaposhauriwa kuwa wavumilivu kusubiri mamlaka husika zikamilishe taratibu za uhamisho wao.




*Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Wilaya ya Singida, wakiwa katika picha ya pamoja nje ya jengo la Ofisi zao. Wa kwanza kushoto ni Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC wilaya hiyo, David Brown, katikati ni Afisa Nidhamu, Boniface Ndege akifuatiwa na Afisa Ajira, Martha Komu.*

Brown anashauri kuwa walimu wanapaswa kuwa wavumilivu na kusubiri hadi pale mamlaka husika zitakapokamilisha taratibu za uhamisho na kuwajulisha hatma ya maombi yao.

Pia, anatoa wito kwa mamlaka inayohusika na kutoa vibali vya uhamisho, kuharakisha mchakato huo ili walimu wasisubiri muda mrefu bila kuwa na majibu.

Kutokana na changamoto hizo, Ofisi ya TSC Singida imejipanga kuongeza nguvu katika kutoa elimu kwa walimu ili kuhakikisha kuwa tatizo la utoro, kughushi nyaraka pamoja na vitendo vingine vya ukiukaji wa maadili ya utumishi wa walimu vinakwisha.

Ofisi hiyo inatarajia kufanya ziara katika shule mbalimbali za Wilaya hiyo hivi karibuni. Ziara hiyo inalenga kukutana na walimu, kutoa elimu juu ya maadili ya kazi ya ualimu, kuwasikiliza na kutatua kero za walimu kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa walimu.

# TSC KILWA YAWANOA WALIMU, WANAFUNZI




*Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC),Wilaya ya Kilwa, Omari Mkuwili, akizungumza na wanafunzi wa shule ya sekondari Miguruwe, alipokuwa katika ziara ya kazi, hivi karibuni.*




*Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC),Wilaya ya Kilwa, Omari Mkuwili (kulia), akizungumza na walimu wa shule ya sekondari Miguruwe (hawapo pichani), alipokuwa katika ziara ya kazi hivi karibuni. Kushoto ni Mkuu wa Shule hiyo, Edina Mmanga.*

**Na Mwandishi wetu**

Tume ya Utumishi wa Walimu, Wilaya ya Kilwa, mkoani Lindi imefanya ziara katika shule za msingi na sekondari za wilaya hiyo na kutoa elimu kuhusu maadili na haki kwa walimu.

Ziara hiyo iliyofanyika Februari 23 hadi 26 mwaka huu, iliongozwa na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC wilayani Kilwa, Omari Mkuwili akiwa ameambatana na msaidizi wake, Esau Kilumbo anayeshughulikia masuala ya ajira na maendeleo ya utumishi wa walimu.

Akizungumza na wanafunzi, Mkuwili aliwasisitiza kujiepusha na mahusiano ya kimapenzi na walimu pamoja na watu wengine ili waweze kufikia malengo yao kielimu.

"Acheni kupanda bodaboda za bure, zina madhara yake. Wewe kila siku unabebwa bure, huyo siyo kaka yako, siyo mjomba wako wala siyo jamaa yako, unafikiri atataka umlipe nini," aliwatahadharisha.

Kwa upande wa maadili kwa walimu, Mkuwili alibainisha kuwa yamejikita katika nguzo kuu tano, ambazo alizitaja kuwa ni pamoja na wajibu wa mwalimu kwa mtoto anayemfundisha.

Nyingine ni wajibu wa mwalimu kwa kazi yake, mwajiri wake, jamii inayomzunguka pamoja na wajibu kwa Taifa lake.

Aidha, alikemea vikali vitendo vya walimu kujihusisha kimapenzi na wanafunzi akisisitiza kuwa "imezuiliwa, imekatazwa na ni maarufuku. Kwa atakayebainika adhabu yake ni kifungo cha miaka 30, kufukuzwa kazi au vyote viwili."

Katika kuonesha uhalisia

# TSC KILWA YAWANOA WALIMU, WANAFUNZI

**"imezuiliwa, imekatazwa na ni maarufuku. Kwa atakayebainika adhabu yake ni kifungo cha miaka 30, kufukuzwa kazi au vyote viwili."**



*Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Wilaya ya Kilwa, Omari Mkuwili, akitoa zawadi kwa Nasra Mkonga, mwanafunzi wa darasa la tano, shule ya msingi Miteja, baada ya kujibu maswali vizuri. Kaimu Katibu Msaidizi Mkuwili alitembelea shule hiyo akiwa katika ziara ya kazi, hivi karibuni.*

wa maneno yake, Mkuwili alitoa mfano wa walimu wanne waliofukuzwa kazi wilayani kilwa mwaka 2020 ambao alisema walibainika kutenda makosa ya kuwa na mahusiano ya kimapenzi na wanafunzi.

Akizungumzia utoaji adhabu kwa walimu wanaobainika kutenda makosa mbalimbali, Mkuwili alisema Tume haifurahii kutoa adhabu kwao isipokuwa inalazimika ili kuwalinda watoto ambao ni tegemeo kwa jamii na Taifa.

Katika hatua nyingine, Kaimu Katibu Msaidizi alitaja makosa mengine ambayo hufanywa na baadhi ya walimu kuwa ni pamoja na utoro.

Akifafanua, alisema baadhi ya walimu hutenda kosa la utoro pasipo wao wenyewe kujua, ambapo alitoa mfano wa kutoroka vipindi darasani, kuondoka kituoni bila ruhusa, kuondoka kwa ruhusa na kuongeza siku za ruhusa, kuacha kazi bila kufuata utaratibu na kushindwa kuhama katika kituo cha kazi baada ya kupata uhamisho.

Vilevile, alisema makosa mengine yanayofanywa na baadhi ya walimu ni pamoja na ulevi wa kupindukia, wizi, na kuhujumu mali za umma. Hivyo aliwaagiza walimu kuepukana na makosa hayo ili wasipoteze ajira zao.

Kwa upande wake, Afisa Ajira Kilumbo aliwaasa walimu kufanya kazi kwa bidii, weledi pamoja na kuzingatia maadili ya taaluma yao kwani ni sehemu ya vigezo vinavyotumika kuwathibitisha kazini.

"Hakikisheni mnafanya kazi kwa bidii na juhudi kubwa bila kujiingiza kwenye mambo yanayoweza kusababisha msithibitishwe kazini," alisisitiza.

Kuhusu upandishwaji vyeo, Kilumbo aliwaeleza walimu husika kuwa ni mchakato ambao unashirikisha idara mbalimbali. Akifafanua, alisema kuwa mchakato huhusisha mwajiri, kisha kupelekwa halmashauri husika na baadaye Kamati ya TSC Wilaya ambayo ndiyo huidhinisha majina yaliyopendekezwa na hatimaye wahusika kupandishwa vyeo.

Katika ziara hiyo, Tume ilifanikiwa kutembelea shule za msingi Matandu, Miteja, Somanga, Singino, Kivinje, Miguruwe, Njinjo na Nangurukuru. Kwa upande wa shule za sekondari zilizofikiwa ni Miguruwe, Njinjo, Nakiu na Kiranjeranje.

# TSC KILWA YAWANOA WALIMU, WANAFUNZI



*Afisa Ajira na Maendeleo ya Walimu kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Wilaya ya Kilwa, Esau Kilumbo akizungumza na wanafunzi wa shule ya sekondari Miguruwe, wakati wa ziara ya kazi hivi karibuni.*



*Baadhi ya Maafisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Wilaya ya Kilwa, wakiwa katika picha ya pamoja na walimu wa shule ya sekondari Njinjo. TSC Kilwa walikuwa katika ziara ya kazi hivi karibuni.*



*Afisa Ajira na Maendeleo ya Walimu kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Wilaya ya Kilwa, Esau Kilumbo (kulia), akidadavua jambo kwa walimu wa shule ya msingi Matandu (hawapo pichani), alipokuwa katika ziara ya kazi hivi karibuni. Kulia kwake ni Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Mwajuma Wakambi.*



*Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Wilaya ya Kilwa, Omari Mkuwili (wa tatu kutoka kulia), akiwa katika picha ya pamoja na walimu wa shule ya sekondari Nakiu, alipokuwa katika ziara ya kazi hivi karibuni.*

# TSC YAADHIMISHA SIKU YA WANAWAKE KWA KUTEMBELEA WATOTO YATIMA



*Afisa Utumishi kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Judith Mtalai akiongea na watoto wa kituo cha watoto yatima cha Nyumba ya Matumani kilichopo Miyuji, Dodoma wakati watumishi wa TSC walipotembelea kituo hicho na kutoa zawadi mbalimbali, Machi 3, 2021.*

**Na Adili Mhina**

Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Machi 3, 2021 walitembelea vituo vya watoto yatima vya Nyumba ya Matumaini na Cheshire Home vilivyopo eneo la Miyuji, jijini Dodoma.

Ziara hiyo iliratibiwa na umoja wa wafanyakazi wanawake wa TSC ikilenga kuwajulia hali watoto wa vituo hivyo pamoja na kuwapatia zawadi ikiwa ni sehemu ya kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, ambayo hufanyika Machi 8 kila mwaka.

Kiongozi wa Msafara huo ambaye pia ni Afisa Utumishi kutoka Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu, Judith Mtalai alieleza kuwa akina mama hao waliamua kuchangishana pesa ili waweze kununua zawadi kidogo kwa ajili ya watoto.

"Tuliona kuwa badala ya kusubiri tarehe 8 Machi na kwenda uwanjani kufurahia siku ya wanawake, ni bora tuanze kwa kuwajali watoto wetu ili nao wajisikie kuwa tupo wazazi tunaowapenda na kuwajali," alisema Mtalai.

Alieleza kuwa zipo changamoto mbalimbali zinazowakabili watoto katika vituo mbalimbali, hivyo watoto hao wanahitaji kuwekwa karibu na jamii kwa kuwasaidia kwa namna mbalimbali ili wasijione wapweke.

"Sisi ni wazazi, tuna watoto na tunalea, hivyo changamoto za watoto walio kwenye vituo





*Picha ya pamoja kati ya watoto wa kituo cha kulelea watoto cha Nyumba ya Matumaini na baadhi ya watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) waliowatembelea watoto hao na kuwapa zawadi, Machi 3, 2021.*

# TSC YAADHIMISHA SIKU YA WANAWAKE KWA KUTEMBELEA WATOTO YATIMA




*Picha ya pamoja kati ya watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu na Mlezi wa kituo cha kulelea watoto cha Cheshire home, Mwl. Getrude Nchubi (Mtawa), wakati watumishi wa Tume walipotembelea kituo hicho na kutoa zawadi, Machi 3, 2021.*

kuwalea watoto.

"Tunasema asanteni sana kwa kujinyima kwenu, kutambua shida za watu wenye matatizo na kuweza kuwasaidia na kuwainua katika hali zao, karibuni tena maana mnatutia moyo, mnatuinua na kutupa nguvu za kuendelea kuwalea hawa watoto, Mungu awabariki na awazidishie pale mlipopunguza," alisema Mwl. Nchudi.

Naye Mkuu wa kituo cha Nyumba ya Matumaini, Aurea Kyara alieleza kuwa kwa sasa kituo hicho kinahudumia watoto 67 ambao wanaanzia umri wa miaka mitatu hadi miaka ishirini na tano na wanasoma madarasa tofauti kuanzia awali hadi ngazi ya chuo.

Aliweka bayana kuwa watoto wote wanagharamiwa na kituo hicho kwa kila kitu huku akieleza kuwa kwa sasa wanakabiliwa na upungufu wa fedha na wameshindwa kuwalipia karo ya shule wanafunzi waliokuwa wanawasomesha katika shule za binafsi.

kama hawa zinatugusa moja kwa moja. Ndiyo maana kwa umoja wetu tumekuja kuwaona na tumewaletea zawadi japo ni kidogo lakini tunaamini zitawasaidia," alisema Mtalai wakati akiongea na watoto wa kituo cha Nyumba ya Matumaini.

Akitoa neno la shukrani mara baada ya kupokea zawadi kwa niaba ya watoto, mwalimu na mlezi wa watoto wa kituo cha Cheshire Home, Getrude Nchudi alieleza kuwa wanafanya kazi katika mazingira magumu, lakini wanapopokea wageni wanaowasaidia watoto, nao pia wanapata moyo wa kuendelea



*Mkuu wa Kituo cha kulelea watoto cha Nyumba ya Matumaini, Aurea Kyara akiongea na watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu - TSC (hawapo pichani), wakati watumishi hao walipotembelea kituo hicho, Machi 3, 2021.*

# TSC YAADHIMISHA SIKU YA WANAWAKE KWA KUTEMBELEA WATOTO YATIMA

"Tumewahamisha wanafunzi wengi wa shule ya msingi kutoka shule za binafsi na tumewasambaza kwenye shule za Serikali kwa kuwa hatuna fedha za kutosha kugharamia karo katika shule za binafsi," alisema Kyara.

Aliwashukuru watumishi wa TSC kwa kuwatembelea huku akieleza kuwa wanakaribisha mtu yeyote anayependa kuwatembelea watoto hao na kwamba siyo lazima kupeleka zawadi ili kuwaona.

"Tunawashukuru sana kwa moyo wenu wa upendo, mnapokuja watoto hawa wanajisikia faraja na wanaona wamezungukwa na jamii ya watu wanaowapenda na kuwajali. Tunamkaribisha mtu yeyote anayependa kuja kuwaona na kuzungumza, siyo lazima hadi awe na zawadi, kuja tu kuwaona ni jambo kubwa kwao," alisema.

Kwa upande wa watoto hao, waliwashukuru watumishi wa Tume kwa kuwatembelea na kuomba watu wengine wenye moyo wa kuwajali wasisite kuwatembelea.

Watumishi wa TSC walikabidhi zawadi mbalimbali ikiwemo sabuni, matunda, vinywaji, mifagio, mpira wa kumwagilia bustani, fedha kwa ajili ya bima ya matibabu kwa watoto wawili wa kituo cha Matumaini pamoja na zawadi nyingine mbalimbali.



*Afisa Utumishi kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Judith Mtalai (kushoto), akikabidhi fedha kwa Mkuu wa Kituo cha kulelea watoto cha Nyumba ya Matumaini, Aurea Kyara, kwa ajili ya kuwakatia bima ya matibabu watoto wawili wa kituo hicho ambao hawakuwa na bima hiyo. Watumishi wa TSC walitembelea Kituo hicho Machi 3, 2021.*



*Kaimu Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Moses Chitama (katikati), akiwa katika picha ya pamoja na wafanyakazi wa Tume hiyo, Makao Makuu, Dodoma.*

**MAWASILIANO:** Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
**Simu: +255 (26) 2322402-4** **Barua Pepe:** *secretary@tsc.go.tz* **Tovuti:** *www.tsc.go.tz*

***Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania*** ***tumeyautumishiwawalimutanzania***